## UHAMISHAJI WA DHAMANA ZA SERIKALI KWA WARITHI

### 1. Ombi la Taarifa za Uwekezaji katika Dhamana za Serikali

**a) Nani anapaswa kuwasilisha:** Msimamizi wa mirathi au Mtekeleza wosia

**b) Mahali pa kuwasilisha:** Benki Kuu ya Tanzania

**c) Nyaraka za kuwasilisha:**

i. **Kwa mirathi iliyotolewa Tanzania:** Nakala ya Hati ya Uthibitisho wa Wosia au Hati ya Teuzi ya Usimamizi wa Mirathi iliyothibitishwa inayomtambua msimamizi.

   **Kwa mirathi iliyothibitishwa nje ya Tanzania:** Nakala hati husika ya uthibitisho inayothibitisha kusajili mirathi Tanzania;

ii. Nakala ya **Cheti cha Kifo** cha marehemu iliyothibitishwa na mamlaka husika;

iii. Kitambulisho cha Msimamizi wa mirathi/Mtekeleza wosia (NIDA, Pasipoti, Kitambulisho cha mpiga kura, au Leseni ya Udereva);

iv. Muhtasari wa kikao kilichomteua Msimamizi wa mirathi/Mtekeleza wosia (ikiwa uteuzi wa usimamizi wa mirathi umefanyika Tanzania).

### 2. Ombi la Uhamishaji wa Dhamana za Serikali kwa Warithi

**a) Nani anapaswa kuwasilisha:** Msimamizi wa mirathi au Mtekeleza wosia

**b) Mahali pa kuwasilisha:** Benki Kuu ya Tanzania

**c) Nyaraka za kuwasilisha:**

i. Barua ya maombi ikieleza:
   a. Kusudio la barua;
   b. Jina la Msimamizi wa mirathi/Mtekeleza wosia;
   c. Mawasiliano ya Msimamizi wa mirathi/Mtekeleza wosia (namba ya simu na barua pepe);
   d. Jina la mwekezaji aliyefariki.

ii. **Kwa mirathi iliyotolewa Tanzania:** Nakala ya Hati ya Uthibitisho wa Wosia au Hati ya Teuzi ya Usimamizi wa Mirathi iliyothibitishwa inayomtambua msimamizi.

   **Kwa mirathi iliyothibitishwa nje ya Tanzania:** Nakala hati husika ya uthibitisho inayothibitisha kusajili mirathi Tanzania;

iii. Nakala ya Cheti cha Kifo kilichothibitishwa;

iv. Nakala ya Hukumu ya Mahakama iliyothibitishwa;

v. Orodha ya mali na hesabu zilizosajiliwa mahakamani;

vi. Orodha ya taarifa za Akaunti za CDS za warithi;

vii. Amri ya Mahakama ya kugawa mali kwa warithi;

viii. Muhtasari wa kikao kilichojadili mgawanyo wa mali za mwekezaji aliyefariki.

Mawasiliano:

Kurugenzi ya Masoko ya Fedha,

Benki Kuu ya Tanzania,

S. L. P 2939,

11884 Dar es Salaam,

2 Mirambo Street,

Simu: +2552233564/3565//3489

Fax: +2552234049

Barua pepe : info@bot.go.tz

Tovuti: https://www.bot.go.tz

**……………………………xx…………………..…………xx……………………………..**